BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika kutekeleza majukumu ya kulijenga taifa letu. Pia, nachukua nafasi hii adhimu kwa moyo wa dhati kabisa, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kutoa maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nichukue nafasi hii kuwatakia afya njema na kuwaombea tahfifu kwa Mwenyezi Mungu wale wote waliofikwa na mitihani ya maradhi ya Corona, maradhi ambayo kwa sasa yanaitikisa dunia na kuacha taharuki mkubwa duniani. Naungana na watu wote wanaoendelea kumuomba Mwenyezi Mungu atuondolee mtihani huu ili tuweze kuendelea na maisha yetu kama kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** naomba pia niwapongeze watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Riziki Juma pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Simai Mohammed Said kwa mashirikiano makubwa waliyokuwa wanaipa Kamati yetu kwa kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi.hii Nachukua nafasi hii kuwaomba watendaji wote wa Wizara waendelee na nidhamu na juhudi ile ile waliyokuwa wanaionyesha Kamati hii kwa Wajumbe wengine wataokuja kufanyia kazi na kuyaendeleza yale ambayo tumeyaacha kwa kuwapa mashirkiano mazuri kwa lengo la kuiimarisha zaidi sekta ya elimu.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii ya Ustawi wa Jamii kwa ushirikiano na michango mikubwa waliyokuwa wanaitoa kwa

Wizara katika Nyanja zote muhimu za sekta ya elimu na hasa katika kuyapitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nichukue fursa hii niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Nassor Salim Ali | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Shehe Hamad Mattar | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Ramadhan Hamza Chande | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Tatu Mohammed Ussi | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Yussuf Hassan Iddi | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Aziza Waziri Kheir | Katibu |
| 9. | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,** Kama tunavyojua kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndiyo chanzo kikuu cha kuzalisha wataalamu wa fani mbali mbali ambao Serikali pamoja na taasisi zisizo za kiserikali zinawatumia katika shughuli mbali mbali za maendeleo ya nchi yetu ambayo upatikanaji wake ni kwa kuongeza bidii na nyenzo madhubuti za kiuchumi pamoja na kuwaendeleza wataalamu wetu katika kada mbali mbali za utumishi wa umma.

**Mheshimiwa Spika,** Elimu bora inapatikana kwa kuzingatia vitu vingi ikiwemo mazingira bora ya kusomea, katika ziara za kazi za kawaida Kamati hii ilishuhudia juhudi za Serikali za kuendeleza ujenzi wa skuli mpya pamoja na kukarabati skuli mbali mbali hasa za zamani ikiwemo Skuli ya Lumba, Haile Selassie na Ben Bella skuli ambazo ni za zamani na zinahitaji ukarabati huo ili mazingira bora ya kufundishia yaweze kuimarika.Kutokana na juhui hizo Kamati inachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake huo ambao ni uamuzi wa busara na umekuja muda muwafaka kwa sasa ambapo skuli hizo zinahitaji matengenezo hayo kutokana na uchakavu katika maeneo yake mengi.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nitoe pongezi za kipekee kwa Mheshimiwa Rais wetu Dr. Ali Mohammed Shein kwa juhudi zake kubwa alizozifanya katika kipindi chote cha uongozi wake za kuziimarisha sekta ya Elimu na Afya. Katika sekta hii ya Elimu, Mheshimiwa Rais alifanya mbali mbali kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanapata elimu inayotolewa kwa Serikali kwa kufanya uamuzi wa kufuta michango waliyokuwa wakichangia wazee wa wanafunzi katika ngazi ya maandalizi, msingi na sekondari. Aidha Serikali pia chini ya uongozi wa Dr. Shein imefanya juhudi za kuimarisha skuli zetu kwa kununua vif mbali mbali vya kusomeshea na kujifunzia. Kamati ya Ustawi wa Jamii inachukua nafasi hii kupongeza kwa dhati juhudi hizo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa afya na nguvu Rais wetu ili aifikishe safari ya uongozi wake salama usalmini.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara y Elimu na Mafunzo ya Amali katika bajeti yenye utekelezaji unaozingatia programu, ina programu kuu sita zenye lengo la kuimarisha sekta ya elimu, programu hizo ni kama ifuatavyo:-

i.) Programu ya Elimu ya Maandalizi na Msingi;

ii.) Programu ya Elimu ya Sekondari;

iii.) Programu ya Elimu ya Juu;

iv.) Programu ya Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali;

v.) Programu ya Ubora wa Elimu; na

vi.) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Elimu.

**Mhweshimiwa Spika**, Kamati ya Ustawi wa Jamii katika ziara zake ilikutana na changamoto mbali mbali ndani ya sekta hii ya elimu changamoto ambazo utatuzi wake ni upatikanaji wa fedha za kutosha. Hivyo, nachukua fursa hii kuiomba Serrikali pamoja na mitijani tuliyonayo ya maradhi ambayo imesababisha kwa kiasi kikubwa kushuka kwa pato letu la taifa, tunaomba fedha zitakapopatikana za kutosha ziongezwe katika bajeti ya Wizara hii.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO WA ELIMU

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Elimu katika kufikia malengo yake ya kunyanyua viwango vya elimu kwa wanafunzi wetu, inapaswa kuweka mipango madhubuti itakayosaidia kufanikisha kwa uimarishaji wa miundoimbinu katika

elimu jambo ambalo litasaidia kutoa huduma bora katika sekta ya elimu na hatimaye kupelekea upatikanaji wa elimu iliyo bora.

**Mheshimiwa Spika**, kazi kubwa ya Wizara ni kuhakikisha kuwa watoto wetu wanapata taaluma ya kutosha itakayoisaidia Serikali kufikia malengo yake ya kuondokana na changamoto ya ukosefu wa elimu iliyo bora, changamoto ambayo Wizara inapaswa kuzidisha juhudi kuiondoa kabisa katika taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa program za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka uliopita kwa kiasi fulani unaridhisha ingawa changamoto nyingi nazo zimekua zikijitokeza lakini kwa kiasi fulani baadhi ya changamoto hizo zimepungua.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Smali kama nilivyoeleza awali ina program kuu sita ambazo utekelezaji wake unahitaji fedha za kutosha ili malengo yaweze kufikiwa. Miongoni mwa mambo yaliyobainika na Kamati wakati wa kupitia bajeti ya Wizara hii katika program zake ni kama ifuatavyo:-

**PROGRAMU YA ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI**

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kuimarisha elimu ya maandalizi na msingi kwa kutoa huduma muhimu zinazohitajika katika vituo vya TuTu kwa kuvipatia ruzuku zitakazowawezesha kutekeleza malengo yote yaliyoapngwa kwa mwaka pamoja na kuimarisha elimu ya msingi hasa katika lugha ya kingereza kwa darasa la kwanza hadi la sita.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ruzuku inayotolewa katika kuviendeleza na kuviimarisha vituo vya TuTu bado kuna changamoto nyingi katika vituo hivyo. Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya vituo hivyo kikiwemo kituo cha TuTu Kisauni ambapo ilijionea changamoto kadhaa ikiwemo ya kutumia jengo la kuazima pamoja na kukosa fedha za kutosha kwa ajili ya kukie desha kituo hicho.

**Mheshimiwa Spika**, nimekitaja kituo hicho kimoja kama mfano lakini vituo vingi vya TuTu vinakabiliwa na changamoto kama hizo jambo ambalo ni kikwazo katika kuviendeleza vituo hivyo wakati vina mchango mkubwa sana katika kuwaandaa watoto wetu kuendelea na masomo yao. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaiomba Wizara katika utekelezaji wa bajeti hii mgao wa fedha uvizingatie kwa umakini vituo vya TuTu.

**Mheshimiwa Spika**, Katika bajeti iliyopita programu hii ilipangiwa jumla ya shilingi 9,010,580,000/-. Hadi kufikia mwezi Aprili 2020 jumla ya shilingi 2,352,438,414/- zilipatikana ambazo ni sawa na 26%. Katika bajeti ya mwaka huu wa 2020/2021 programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 6,326,127/-.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Ustawi wa Jamii inaamini kuwa endapo fedha hizi zitapatikana kwa wakati na zitagaiwa kama zilizvyopanga, baadhi ya changamoto ambazo Kamati ilizikuta zitaondoka. Aidha tunaiomba Wizara ijitahidi kuifanyia kazi bajeti hii kwa kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati.

**PROGRAMU YA ELIMU YA SEKONDARI**

**Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa malengo ya programu ni kuimarisha mazingira ya kusomea kwa wanafunzi, Kamati ya Ustawi wa Jamii ilipokua katika ziara zake za kawaida ilifanya ziara katika skuli mbali mbali za sekondari na kujionea changamoto kadhaa ambazo baadhi yao kama nilivyoeleza huko juu kuwa zimneanza kufanyiwa kazi kwa kukarabatiwa na Kamati inapongeza sana juhudi hizo na tunaomba ukarabati huo ukamilike kwa wakati uliopangwa. Katika ziara hiyo Kamati ilikutana na changamoto nyingi katika skuli hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika skuli nyingi za sekondari hapa nchini, kuna changamoto kubwa ya kukosekana kwa maabara zilizokamilika na maktaba jambo ambalo ni changamoto kwa wanafunzi. Kutokana na haki hiyo, Serikali imeamua kujenga **"School Hubs"** kwa baadhi ya maeneo jambo ambalo ni jema na Kamati inapongheza sana uamuzi huu wa Serikali. Pamoja na kujengwa kwa **"School Hubs"** hizo Kamati inaiomba Serikali kuhakikisha kuwa inajipanga kwa kutoa bajeti ya kutosha kwa ajili **"School Hubs"** ili ziweze kutoa huduma inayokosekana katika skuli za maeneo ya karibu.

**Mheshimiwa Spika**, Katika bajeti iliyopita programu hii ilipangiwa jumla ya shilingi 94,195,379./=. Hadi kufikia mwezi Aprili 2020 jumla ya shilingi 57,636,099,604/= zilipatikana ambazo ni sawa na 55%. Katika bajeti ya mwaka huu wa 2020/2021 programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 58,124,505/=.

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri fedha kwa ajili ya matumizi ya program hii zimeongezeka kidogo, hivyo tunaiomba Wizara ijipange vizuri kwa ajili ya kutekeleza shughuli zote zilizopangwa kikamilifu ikiwemo ununuzi wa vifaa vya maabara kwa skuli zinazokabiliwa na changamoto hiyo pamoja na **"School Hubs"** mpya zote zinazojengwa na Serikali.

**PROGRAMU YA ELIMU YA JUU**

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii ni mniongfoini mwa programu zinazohitaji fedha nyingi kwa kuzingatia kuwa inalenga kusaidia uzalishaji wa wataalamu mbali mbali ambao ndio ngao ya mae deleo ya nchi yetu. Wizara ina majukumu makubwa yakiwemo ya kusimamia upatikanaji mzuri wa fedha zitakazoisaidia Bodi yake ya Mikopo ya Elimu ya juu kutoa mikopo kwa wakati kwa wahitaji wote.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu ilifanya ziara katika baadhi ya taasisi ambazo utekelezaji wa malengo yakwe unategemea sana fedha za program hii. Miongoni mwa maeneo ambayo yalitembelewa na Kamatgi ni pamoja na Chuo cha Kiislamu Mazizini na Chuo cha Kiislamu Micheweni ambapo kuna chanhgamoto kadhaa ambazo zinahitaji fedha ili ziweze kutatuka. Katika Chuo cha Kiislamu Micheweni Kamati ilikuatana na changamoto nyinvi ambazo tumezileleza kwenye ripoti yetu kwa urefu zaidi lakini kubwa ambalo Kamati inaiomba Wizara katika Bajeti inayokuja ilifanyie kazi ni suala la ujenzi au ukarabati wa dakhalia za wanafunzi. Kamati katika ziara zakwe ilitembelea maeneo hayo na kukutana na halki isiyoridhisha ya kuvuja na kuchakaa kwa majengo wanayiotumia wanafunzi kwa sasa, hivyo tunaomba bajeti ijayo suala hilo lizingatiwe.

**Mheshimiwa Spika,** suala la ubunifu katika baadhi ya taasisi zilizo chini ya program ni la kuzingatiwa kwa lengo la kuongeza mapato ambayo yatasaidia utekelezaji wa malengo yaliyopangwa chini ya mwamvuli wa program hii. Naomba kuchukua nafasi hii kuvishauri vyuo vikuu ambavyo vina nafasi ya kujiongezea mapato kupitia utaratibu wa masomo ya muda mfupi “short course” ili fedha hizo zitakapopatikana zitumike katika kutatua changamoto za vyuo hivyo ikiwemo changamoto ya makaazi ya wanafunzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Ustawi wa Jamii inaiomba Serikali kuangalia upya vipaumbele vyake vya bajeti na kutosahau umuhimu wa elimu katika jamii yetu kutokana na ukweli kwamba nchi yoyote ile duniani hujengwa na wataalamu ambao hawapatikani kwa njia nyengine zaidi ya kuwaendeleza kimasomo.

**Mheshimiwa Spika;** Serikali kwa nia njema iliamua kuziunganisha baadhi ya taasisi na Chuo Kikuu cha Taifa, bado kuna changamoto nyingi katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo pamoja na malalamiko ya kukosekana kwa fedha za ruzuku za kujiendesha kwa taasisi hizo. Kamati ilifanya ziara katika

baadhi ya taasisi na kuendelea kupokea malalamiko hayo ambayo yapo tokea taasisi hiziu zilipoungana. Hivyo, napenda kuchukua nafasi hii kuiomba Serikali kuzidisha juhudi zake kwa kutoa fedha za ruzuku ili ziweze kujiendesha pamoja na kutekeleza majuku yake kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** katika bajeti iliyopita, program hii ilipangiwa jumla ya shilingi 9,097,474/-, fedha ambazo zimetumika kwa kuzigawa katika program ndogo tano ambazo ni program ndogo ya mafunzo ya ualimu, huduma ya elimu ya juu, ushauri na utafiti, huduma ya sayansi na teknolojia, huduma ya mikopo ya elimu ya juu na huduma ya uratibu wa elimu ya juu.

**Mheshimiwa Spika**, Programu ndogo ya Mafunzo yan Ualimu ilitengewa jumla ya shilingi 1,013,667,000/-. Hadi kufikia Mwezi Aprili 2020, jumla ya shilingi 642, 470, 415/- zilipatikana sawa na 63%. Kwa upande wa Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti kupitia Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), ilitengwa ruzuku ya shilingi 11,239,100,000/-. Hadi kufikia mwezi Aprili 2020, jumla ya shilingi 10,666,409,562 zilipatikana ambazo ni sawa na 95%. Kwa upande wa Huduma ya Sayansi na Teknolojia kwa bajeti iliyopita kupitia Taasisi ya Karume ya Sayansi ilitengewa ruzuku ya shilingi 1,626,000,000/-. Hadi kufikia mwezi Aprili 2020, jumla ya shilingi 1,393,132,060/- ambazo ni sawa 86%.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upandewa Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa bajeti iliyopita ilitengewa jumla ya ruzuku ya shilingi 10,298,600,000/-. Hadi kufikia mwezi Aprili 2020, jumla ya shilingi 6,706,532,312 zilipatikana ambazo ni sawa na 65%. Kwa upande wa Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu kwa bajeti iliyopita jumla ya shilingi 50,000,000/- zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa huduma hii. Hadi kufikia mwezi Aprili 2020, jumla ya shilingi 28,000,000/- zilipatikana ambazo ni sawa na 56%.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa bajeti ya mwaka huu wa 2020/2021, programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 30,424,556/-.

**PROGRAMU YA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI**

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kutoa elimu ya mafunzo ya amali na elimu mbadala kwa wanafunzi kulingana na mahitaji ya soko la ajira pamoja na kuwapa mbinu mbadala za kuweza kujiajiri wenyewe. Programu hii ina Program ndogo mbili zote ambazo ni program ndogo ya Mafunzo ya Amali na Program ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima.

**Mheshimiwa Spika,** program hii inailenga kutoa mbinu na elimu mbadala kwa kutoa ujuzi utakaomuwezesha mwanafunzi kujiajiri na hatimae kuipunguzia mzigo na lawama Serikali. Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuanzisha program hii, bado Kamati inasisitiza uingizwaji wa fedha za kutosha katika program hii ili malengo yaliyopangwa yaweze kukamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokuwa katika ziara zake ilitembelea maeneo mbali mbali katika vyuo vya Amali na katika skuli ya Elimu Mbadala Rahaleo na kujionea juhudi mbali mbali za Serikali zinazochukuliwa kuziendeleza skuli na vituo hivyo. Hata hivyo, Kamati ilikutana na changamoto ya baadhi ya walimu kulalamikia kucheleweshwa kwa fedha za matumizi yao jambo ambalo huwalazimu kutumia fedha zao kununua vifaa hivyo. Kutokana na malalamiko hayo, Kamati inaiomba Serikali kujitahidi kuingiza fedha hizo kwa wakati ili mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi yafanyike bila ya kuwa na kuzuwizi chochote.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia hotuba hii Kamati inaipongeza sana Serikali kwa juhudi zake mbali mbali inazochukua katika kuimarisha sekta ya Elimu. Katika kipindi chote cha uongozi wa Rais wetu Dr. Ali Mohammed Shein, tumeshuhudia kwa vitendo juhudi kubwa za kuimarisha sekta hii ikiwa ni pamoja na kusimamia vyema ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Amali kilichopo Makunduchi ambacho ujenzi wako awali ulizorota lakini kwa sasa baada ya mikakati mbali mbali iliyochukuliwa na Wizara na Serikali kwa ujumla, ujenzi huo upo katika hatua nzuri sana na tunachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali pamoja na Rais wetu. Kamati ya Ustawi wa Jamii inaamini kuwa kutokana nakasi iliyoikuta wakati wa ziara zake, chuo hicho hakina muda kitaanza kutumika ili vijana wetu waweze kujipatia ujuzi utakaowasaidia kujiendeleza kimaisha na kuondoa lawama zaukosefu wa ajira miongoni mwa vijana hao.

**Mheshimiwa Spika**, Programu ya Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali kama nilivyosema hapo awali ina Programu ndogo mbili ambazo zote hupatiwa ruzuku kwa lengo la kujiendesha na kusaidia utekelezaji wa malengo yaliyopangwa. Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali kwa mwaka uliopita ilitengewa jumla ya ruzuku ya shilingi 7,761,200,00/-, hadi kufikia mwezi Aprili 2020, jumla ya shilingi 4,916,633,665/- ambazo ni sawa na 63% zilipatikana. Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima kwa mwaka uliopita ilitengewa shilingi 8,974,245,000/-, hadi kufikia mwezi Aprili 2020, jumla shilingi 5,877,186,531/- sawa na 66% zilipatikana. Kwa mwaka huu wa fedha program hii

imepangiwa jumla ya shilingi 9,366,839/-, ambazo Kamati yangu inaamini kuwa endapo zitapatikana kwa wakati zitasaidia kuondoa baadhi ya changamoto zilizopo katika program hii.

**PROGRAMU YA UBORA WA ELIMU**

**Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la programu hii ni kutoa elimu bora kwa ngazi zote za elimu. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndiyo daraja la kuvukisha taaluma na hamtimaye kupelekea upatikanaji wa huduma bora zinazotolewa na taasisi za Serikali na sekta binafsi kuwafikia wananchi wetu. Programu hii imezidi kuimarika kutokana na juhudi kubwa za Serikali zinazochukuliwa ambapo katika kipindi cha miaka tisa ya uongozi wa Dr. Ali Mohmammed Shein, Serikali imeweza kuongeza idadi ya skuli za maandalizi na msingi zinazopatiwa chakula kutoka skuli kumi mwaka 2014 hadi kufikia skuli 27 mwaka 2019.

**Mheshimiwa Spika,** tunaamini kuwa hatua hii ni kubwa sana katika kuweka ubora mzuri wa viwango vya elimu hapa nchini kutokana na ukweli kwamba watoto wetu wanaweza kusoma wakiwa na afya na utulivu wa akili. Aidha, Serikali imefanya juhudi mbali mbali za kuongeza idadi ya vikalio katika skuli zetu jambo ambalo lilikuwa ni changamoto kubwa sana.

**Mheshimiwa Spika**, Miongoni mwa majukumu ya program hii ni pamoja na kuandaa huduma ya mitaala na vifaa vya kufundishia kwa ngazi ya elimu ya maandalizi, msingi, sekondari na katika mafunzo ya ualimu. Katika ziara za Kamati tulipata malalamiko kadhaa kutoka kwa baadhi ya wadau wa elimu wakidai kuwa baadhi ya skuli za binafsi hazifuati mitaala yetu jambo linalopelekea kuwachanganya wanafunzi na baadhi yao kutofanya vizuri katika mitihani ya kitaifa. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa kuna baadhi ya skuli hizo za binafasi zinachagua wanafunzi kwa kuwachukua wanafunzi wenye uwezo tu na wale wanaohisi uwezo wao wa kufaulu ni mdogo huwaacha na kuwatekeleza katika kipindi ambacho wanafunzi wanahitaji msaada wao ili waweze kufanya vizuri katika masomo yao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inachukua nafasi hii kuiomba Wizara ya Elimu kupitia Taasisi ya Elimu Zanzibar ambayo ndie msimamizi mkuu wa mambo hayo kudhizibiti skuli zote za binafsi ambazo hazifuati utaratibu uliowekwa na Serikali. Pia tunaiomba Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu kuzikagua kwa umakini skuli za binafsi ili baadhi ya changamoto ambazo zinalalamikiwa ziweze kuondoka.

**Mheshimiwa Spika**, ili majukumu hayo mazito yaweze kutekelezwa fedha za kutosha zinahitajhika ili watendaji wa taasisi zilizo chini ya mwamvuli wa program hii waweze kutimiza wajibu wao. Hivyo, Kamati ya Ustawi wa Jamii inachukua nafasi hii kuiomba Serikali kuongeza ruzuku kila fedha inaporuhusu kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** ubora wa elimu hauwezi kuaptikana pasipokuwa na usimamizi mzuri wa kufanya ukaguzi katika skuli zetu zote za Serikali na binafsi, Kamati ya Ustawi wa Jamii inarudia tena ombi lake kwa Wizara, kufanya ukaguzi wa mara mara katika skuli za Serikali na inapendekeza ukaguzi kwa skuli za Serikali ufanyike kwa kuwapeleka wakaguzi watakaotoka maeneo tofauti na eneo linalokaguliwa, jambo hili litapelekea ufanisi mkubwa katika kazi za ukaguzi maskulini. Kamati pia inaiomba Wizara iwanunulie nyenzo za kufanyia kazi wakaguzi wote ili kuwaondolea usumbufu unaojitokeza kwa baadhi ya wakaguzi kukosa vitendea kazi ikiwemo usafiri.

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii katika utekelezaji wake imejigawa katika maeneo matano ya kutoa huduma ambayo ni huduma ya mitaala na vifaa vya kufundishia, huduma ya upimaji na tathmini ya elimu, huduna ya ukaguzi wa elimu, huduma za maktaba na huduma ya urajis wa elimu. Kila kipengele cha utoaji wa huduma kipangiwa fedha zake za bajeti katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** katika bajeti iliyopita, huduma ya mitaala na vifaa vya kufundishia kupitia Taasisi ya elimu, ilipangiwa ruzuku ya shilingi 573,100,000/=. Hadi kufikia Aprili 2020, jumla ya shilingi 503,978,320/- zilipatikana sawa na 88%. Pia huduma ya upimajia na tathmini ya elimu kupitia Baraza la Mitihani Zanzibar kwa mwaka uliopita ilipangiwa ruzuku ya shilingi ya shilingi 4,941,800,000/=, hadi kufikia mwezi Aprili 2020, jumla ya shilingi 4,319,112,010/- sawa na87% zilipatikana. Huduma ya ukaguzi wa elimu chini ya Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu kwa mwaka ulipita ilipangiwa jumla ya ruzuku ya shilingi 1,090,500,000/-. Hadi kufikis mwezi Aprili 2020, jumla ya shilingi 809,277,751/- sawa na 745 zilipatikana.

**Mheshimiwa Spika**, huduma za maktaba chini ya mwamvuli wa Shirika la Maktaba kwa mwaka uliopita ilipangiwa ruzuku ya shilingi 886,200,000/-. Hdi kufikia mwezi Aprili 2020, jumla ya shilingi 586,049,457/- sawa na 66% zilipatikana. Huduma za urajis wa elimu kupitia Ofisi ya Mrajis wa Elimu kwa mwaka ulipita ilipangiwa kutumia ruzuku ya shilingi 249,600,000/-. Hadi kufikia mwezi Arprili 2020, jumla ya shilingi 192,966,950 zilipatikana sawa na 77%.

**Mheshimiwa Spika**, program hii pia ina program ndogo tatu ambazo ni program ndogo ya michezo na utamaduni katika skuli, program ndogo ya teknolojia ya habari na mawasiliano na na program ndogo ya elimu mjumjuisho na stadi za maisha.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue fursa hii kuiomba Seriali kupitia bajeti hii kupanga mipango madhubuti ya kukiendeleza kitengo cha Elimu Mjumuisho na DStadi za Maisha kwa kukipatia fedha ya kutosha na kwa wakati kieze kujiendesha pamoja na kutatua changamoto nyingi ambazo zipo katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, programnu hii kwa mwaka ujao wa 2020/2021 programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 10,189,493/-, tunaomba fedha hizi zipatikane kwa wakati ili malengo yaliyopangwa yaweze kutimizwa.

## 6. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ELIMU

**Mheshimiwa Spika,** program hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa nyenzo zilizo bora zinapatikana na zinatumika kwa lengo la kuimarisha utoaji na upatikanaji wa huduma ya elimu nchini. Uendeshaji na uratibu wa shughuli za elimu ni jambo muhimu sana hasa tukizingatia kuwa nchi yetu inaundwa na visiwa viwili ambapo huduma ya elimu inahitajika katika visiwa vyote.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara zetu za kawaida za Kamati tuligundua changamoto nyingi sana kisiwani Pemba jambo ambalo hupelekea baadhi ya wakati kutokamilika kwa malengo yaliyopangwa na Wizara, hivyo tunaiomba Serikali kuongeza fedha katika program hii ili changamoto nyingi ambazo baadhi yao hazihitaji nguvu ya ziada ziweze kutatuka.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka uliopita Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Elimu ilipangiwa jumla ya shilingi 14,599,201,000.kwa mwaka huu wa fedha wa 202012 programu hii imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 24,972,498/-, fedha ambazo zimekusudiwa kutumika katika kuzisaidia taasisi zote zilizo chi l ya programu hii.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii katika Baraza lako

tukufu, pia niwashukuru Wajumbe wako kwa utulivu wao waliouonesha wakati nawasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Nawaomba Wajumbe wako waichangie bajeti hii, wahoji na watoe mapendekezo yao panapohitajika na hatimaye kuipitisha baada ya kuafikiana kwa hoja mbali mbali watakazoibua wakati wa mjadala.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

……………………………………..

**Mwanaasha Khamis Juma,**

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Ustawi wa Jamii,**

**Baraza la Wawakilishi,**

**Zanzibar.**